**SOMO LA 7**

**Ufahamu unakupa nuru ya ukweli wa Biblia**

**MAFUNZO YA BIBLIA KUHUSU ASIILI YA BINADAMU**

“Kwa maana Yeye anatujua umbo letu, na kukumbuka ya kuwa sisi tu mavumbi. Mwanadamu siku zake zi kama majani; kama ua la kondeni ndivyo astawivyo. Maana upepo hupita juu yake, kumbe haliko! Na mahali pake hapatalijua tena” (Zaburi 103:14-16)

“Ufunguo” unaofuatia ni ule wa kufungua mafundisho ya maandiko na kuelewa yanavyosema kuhusu asili ya binadamu. Tusipofahamu mafunzo ya kimsingi ya maandiko kuhusu maumbile ya mtu, hatutaweza kuufahamu ukweli kuhusu kazi na mafunzo ya Kristo, aliyekuja kufungua na kuonyesha njia ya kupata uzima wa milele, ambao ni ahadi ya karama ya Mungu.

Maoni ya walimwengu na dhana ya maumbile ya mwanadamu ni kuwa kuna kitu ndani ya mwili wa mtu isiyokufa – kitu ambacho kitaendelea kuishi baada ya mwili kupatikana na mauti. Istilahi inayotumika kwa “kitu” hiki ni “soul”-nafsi, “immortal soul” – “roho isiyokufa.” Katika somo hili tutaona kuwa ingawa maneno “immortal” – “isiyopatikana na mauti” na “soul”- “roho” yanapatikana katika Biblia, hayatumiwi pamoja kamwe, au katika kifungu au mlango mmoja. Kwa hakika, “Immortal” – “asiyeona uharibufu” yaonekana mara moja tu katika maandiko na ikimhusisha Mungu (1 Timotheo 1:17)

Kwa hivyo, Biblia yasema nini kuhusu “roho” (soul)? Ufafanuzi wa maandiko kuhusu ”soul” – “roho” ni nini?

Tafadhali rejelea Somo la 4 ambapo tuligusia vitabu vya marejeleo vinavyoweza kutusaidia katika kufahamu Biblia, kwa sababu Kiswahili haikuwa lugha ya asili. Ni jambo la kuvutia kuangalia neno hili kwa Kiingereza kwa kutumia Strongs Concordance – Marejeleo ya Bwana Strong, ambapo twapata maneno ya asili yaliyotafsiriwa “nephesh” kwa Kiebrania na “psuche” kwa Kiyunani.

Tukiwa na ufahamu huu twaweza kufuatiia istilahi hii “nephesh” na “psuche” katika lugha ya Kiingereza na vitabu vya marejeleo katika lugha ya Kiebrania na Kiyunani, ambapo yanaorodhesha kwa mpango neno la asili hilo linapotokea. Kwa nini tujishughulishe na zoezi hili? Tutathibitisha ya kuwa hakuna mahali popote katika Biblia nzima tunapoweza kupata maelezo ya: “never-dying-soul” – “roho isiyopata uharibifu,” “immortal soul” – “roho isiyokufa” au “immortality of the soul” – “kuishi  milele kwa roho.” Kinyume na haya, tutapata mambo tofauti kabisa. Tutapata ya kuwa maandiko yanaeleza kwa wingi na ushawishi sufufu maisha mafupi ya kuishi kwa mwanadamu.

Matumizi ya neno “soul” – “roho” bila shaka yatuamulia msingi wake . Twapata neno “soul” - ”roho”(Kiebrania nephesh; Kiyunani psuche) si zaidi ya kiumbe anayepumua bila kurejelea muda wa kuishi kwake.

Katika Mwanzo 1 na 2, maneno ya asili yanayomwelezea mnyama na mwanadamu ni SAWA (chay nephesh). Inayonenwa juu ya huyu ndiyo inayonenwa kwa mwingine. Kwa mfano:

"Mungu akaumba …kila kiumbe chenye uhai (chay nephesh) kiendacho" (Mwanzo 1:21)

"Nchi na izae kiumbe hai (chay nephesh)" (Mwanzo 1:24).

Vifungu hivi vinazungumzia kipekee juu ya wanyama, kabla ya mtu kuumbwa. Nephesh inapotokea mara 4 mwanzoni (ikitafsiriwa "kiumbe" na "hai") inawahusu wanyama (Mwanzo 1:20,21,24,30).

Sasa tafadhali angalia yanayosemwa kuhusu kuumbwa kwa mwanadamu –

"BWANA Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia (neshamah) puani pumzi ya uhai (neshamah chay); mtu akawa nafsi hai (chay nephesh)." (Mwanzo 2:7)

Twaona kuwa maneno yanayotumiwa kumwelezea mnyama na mwanadamu ni mamoja – ingawa katika kutafsiri tuna "living creature" – "kiumbe hai" na "living soul" – "nafsi hai." Yote ni viumbe hai, viumbe wenye uhai. Lakini hakuna katika Kiebrania asili wazo la kiumbe aliye na uhai wa milele. Kama kunao, basi tungelazimika kukubali hali iyo hiyo kwa watu na wanyama. Maumbile yao ya kimsingi ni mamoja – hali na mwili.

Katika mwanzo 2:7, tumeonyeshwa ya kuwa Adamu aliumbwa kwa mavumbi ya ardhi; na alipopuliziwa pumzi puani, YEYE (umbo la mavumbi) akawa "nafsi hai," kiumbe mwenye uhai. Kitu hicho kilichokuwa mavumbi akawa (sio akapokea) nafsi hai au kiumbe hai, sawa na wanyama wale wengine.

Biblia yatwambia ya kuwa roho au nafsi (soul) yaweza kuhisi njaa, yaweza kushiba chakula –

"Na nafsi (nephesh) yake mvivu itaona njaa "  (Mithali 19:15).

"Wameyatoa matamaniko yao wapate chakula cha kuihuisha nafsi (nephesh)" (Maombolezo 1:11)

Roho/nafsi zaweza kwenda kaburini, na kupanda kutoka huko –

"Naam, nafsi (nephesh) yake inakaribia shimoni" (Ayubu 33:22)

"Yeye ameikomboa nafsi(nephesh) yangu isiende shimoni (Sheol kwa Kiebrania ni kaburi)" (Ayubu 33:28)

"Umeniinua nafsi (nephesh) yangu, Ee Bwana, kutoka kuzimu(kaburi)" (Zaburi 30:3)

Neno hili nephesh limetokea mara 750. Imetafsiriwa "soul"470, "hai" mara 120, "mtu" mara 30. Imetaja wanyama pekee mara 22, na kujumuisha watu na wanyama mara 7. Pia imetafsiriwa kama mtu, nafsi, mnyama, samaki, kiumbe, mwili, moyo, hamu (ya kula) n.k.

Haisemwi kama ni kitu cha kuishi milele popote: ni kinyume na hilo kila wakati. Mara zaidi ya 300 yasemekana kama yaweza kufa, kimaumbile yaweza kufa, yauawa (mara 32), ikiwa hasa imekufa (mara 13), ikielekea kaburi/kuzimu (mara 13)

Kwa mfano:

“Naam, yeye asiyeweza kujihuisha nafsi(nephesh) yake” **(**Zaburi 22:29 **)**

“Atakayejiokoa nafsi (nephesh) yake mkono wa kuzimu?” (Zaburi 89:48)

“Wala hakuziepusha roho (nephesh) zao na mauti” (Zaburi 78:50)

Ezekieli anatoa kauli:”Roho ile itendayo dhambi itakufa” (Ezek. 18:4)

Walawi 24:17-18 inafunua bayana – “Na mtu ampigaye mtu (nephesh) hata akafa, lazima atauawa; na atakayempiga mnyama(nephesh) hata akafa atalipa uhai kwa uhai(nephesh)”

Mwishowe Biblia yazungumzia “souls” roho kuwa zimekufa hasa –

“Asikaribie maiti (nephesh)” (Hesabu 6:6)

“Wala hataingia penye maiti (nephesh) ” (Walawi 21:11)

Taswira au picha iyo hiyo twaiona katika Agano Jipya (ambapo neno lenye maana sawa katika lugha ya Kiyunani lapatikana, “Soul” – “roho” ni psuche)

“Wakafa theluthi ya viumbe vilivyomo baharini, vyenye uhai(psuche) “ (Ufunuo 8:9)

“Na vitu vyote vyenye roho (psuche) ya uhai katika bahari vikafa” (Ufunuo 16:3)

“Watu waliohatarisha maisha (psuche) yao kwa ajili ya jina la Bwana wetu Yesu Kristo (Matendo 15:26)

“Lakini siyahesabu maisha (psuche) yangu kuwa kitu cha thamani kwangu”(Matendo 20:24)

“Maana kwa ajili ya Kristo alikaribia kufa akaponza roho (psuche) yake” (Wafilipi 2:30)

Kujaribu kutafsiri “psuche” kwa kuweka “immortal soul” – roho inayoishi milele sehemu yoyote hapo juu itashangaza sana. Paulo anaiweka wazi kuwa “nafsi hai” ni “mwili wa asili” anaposema:

“Uko mwili wa asili(psuchikon kutokana na psuche:roho) na wa roho (pneumatikon) pia uko. Ndivyo ilivyoandikwa mtu wa kwanza, Adamu akawa nafsi iliyo hai (psuche); Adamu wa mwisho ((Yesu) ni roho (pneuma)” (1 Kor 15:44)

Maandiko yanaonyesha wazi kuwa, mbali na kujiona kuwa yeye ni sehemu ya asili ya Mungu anayeshi milele, mtu wa kawaida aliye kama mnyama asiyeongozwa kwa amri za Mungu, ni kitu bure kabisa.

“Na watu wote wanaokaa duniani wanahesabiwa kuwa si kitu” (Danieli 4:35)

“Binadamu amefanana na ubatili, siku zake ni kama kivuli kipitacho” (Zaburi 144:4)

“Uzima wenu ni nini? Maana ninyi ni mvuke uonekanao kwa kitambo, kisha hutoweka” (Yakobo 4:14)

Hakuna kitu kinachoonyesha katika Biblia kuwa kuna tofauti baina ya mtu na mwili wake, au kuonyesha kuwa mtu anaweza kuishi pasipo kuwa na mwili wake. Tumeona ya kuwa Mungu alimfanya mtu (mwenyewe) kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani pumzi yenye uhai na “MTU akawa nafsi hai “ au kiumbe hai. Hayo mavumbi yakawa kiumbe hai.

Ni bayana kuwa mwili uliotokana na mavumbi ndio unaorejelewa hapa. Mungu hakupuliza ndani ya mwili huu “nafsi hai.” Haisemi hivyo. Inasema, pumzi yenye uhai – aliyompulizia – ilifanya yale mavumbi yaliyoumbwa kuwa mtu, nafsi hai.

Kwa sababu ya kutotii amri ya Mungu, Adamu (mavumbi haya yaliyofanyika mtu) alihukumiwa kurudi ardhini  (Mwanzo 3:17-19)

“Hata utakapoirudia ardhi ambayo katika hiyo ulitwaliwa; kwa maana U mavumbi wewe, NAWE mavumbini utarudi.” (Mwanzo 3:19)

Mtu huyu alitajwa hapa kama “U” na “NAWE,” huyo mtu mkosaji. Ibrahimu naye alisema hivi kujihusu:

“Nami ni mavumbi na majivu tu (MWanzo 18:27).

Mtu hufa kama vile mnyama wa kondeni. Miili yao ni sawa. Kama ambavyo tumeona, waliumbwa katika hali moja, twapata kuwa wanakufa katika hali moja –

“Na tazama, nitaleta gharika ya maji juu ya nchi niharibu KILA KITU chenye mwili na pumzi ya uhai (ruach chaiyim)”(Mwanzo 6:17)

“Wakafa WOTE wenye mwili waendao juu ya nchi, na ndege, na wanyama wa kufugwa, na kila mnyama wa mwitu, na kila kitambaacho chenye kutambaa juu ya nchi, na kila mwanadamu. Kila kitu chenye pumzi ya roho ya uhai puani mwake kikafa, kila kilichokuwako katika nchi kavu” (Mwanzo 7:21-22)

Suleimani anaongeza neno adilifu la Mungu –

“Kwa maana linalowatukia wanadamu linalowatukia wanyama; jambo moja lawatukia; anavyokufa huyu ndivyo anavyokufa huyu; naam, WOTE WANAYO PUMZI MOJA (ruach:

roho, neno moja). Wala mwanadamu hana kitu cha kumpita mnyama… Wote huendea mahali pamoja; wote hutoka katika mavumbi; na hata mavumbini hurudi tena" (Mhubiri 3:18-20).

"Nayo mavumbi kuirudia nchi kama yalivyokuwa. Nayo roho (ruach, pumzi) kumrudia Mungu aliyeitoa"(Mhubiri 12:7)

Hii kuwa ni roho au pumzi ambayo ni yake Mungu na inaijaza sehemu yote, na sio kitu hai cha kibinafsi cha kumrudia Mungu wakati wa kufa, yathibitisha kuwa huwahusisha wanyama pia kama inavyoonekana katika zaburi 104: (Angalia muktadha wote)

"Ndimo mlimo viendavyo visivyohesabika, viumbe hai vidogo kwa vikubwa… Hao wote wanakungoja Wewe, uwape chakula chao kwa wakati wake… Waiondoa pumzi (ruach:spirits pumzi) yao, wanakufa, na kuyarudia mavumbi yao."

Na katika kitabu cha Ayubu twasoma –

"Kama akimwekea mtu moyo wake, akijikusanyia roho yake na pumzi yake; wenye mwili wote wataangamia pamoja, nao WANADAMU watarejea tena kuwa mavumbi" (Ayubu 34: 14-15 )

Hapa tena twaona bayana kuwa roho au pumzi ikikusanywa ni ya Mungu, ni MWANADAMU mwenyewe anayerudi mavumbini hatimaye . Kama ingelikuwa kweli eti mtu ana roho isiyoweza kufa, na wakati wa kufa hiyo roho yaenda kukaa na Mungu milele, haya tuliyosoma hayangekuwa na mashiko yoyote ; maelezo haya yangekosa nguvu. Ingemaanisha kuwa Mungu anapokusanya pumzi yake, wenye miili wote hawaangamii kabisa na pia mtu hangerudi mavumbini kama maelezo hayo yanavyoonyesha kwa mkazo na muktadha unavyotaka tuelewe.

Tuliona Suleimani akisema, "Mwanadamu hana kitu cha kumpita mnyama" (kwa maumbile yake asili na mwili wake ulivyoumbwa). Daudi pia anasema:

"Lakini mwanadamu hadumu katika heshima, bali amefanana na wanyama wapoteao" (Zaburi 49:12)

**MASWALI ya somo la 7**

1. Maana ya kimsingi ya neno "soul" – "roho" ni nini kama inavyotumika katika Biblia?
2. Istilahi gani imetumiwa katika mwanzo 1:20 & 24 kuelezea wanyama walioumbwa?
3. Istilahi gani imetumiwa katika Mwanzo 2:7 kuelezea mtu aliyeumbwa?
4. Maneno yapi ya Kiebrania yametumiwa katika Mwanzo 1:20-21, Mwanzo 1:24, Mwanzo 1:30; Mwanzo 2:7 kwa "living soul" – "nafsi hai" na "kiumbe hai"?
5. Je, watu na wanyama wanaelezwa (kimwili) na Mungu kama ni sawa?
6. Je, kuna chochote ambacho kinasheheni wazo la kitu kisichoweza kufa katika maneno ya awali Biblia inapotaja "living soul" – "nafsi hai" na "living creature" – "kiumbe hai" ?
7. Adamu aliumbwa kutokana na nini?

8. Je, roho yaweza kufa? Toa vifungu viwili vya maandiko kuthibitisha jibu lako.
9. Mungu anawachukuliaje wote wasiothamini amri zake?
10. Je, Biblia inaonyesha tofauti yoyote kati ya mtu na mwili wake?
11. Katika kuumbwa kwa mtu, ni nini kilichofanyika "ikawa kiumbe hai"?
12. Nini hufanyika mtu anapokufa?
13. Ibrahimu alijieleza aje katika Mwanzo 18:27?
14. Nakili vifungu vya kuonyesha wanyama na watu wote wana pumzi moja ya uhai.
15. Je, kuna tofauti yoyote baina ya mtu na wanyama kuhusu maumbile ya kimwili? Jaribu kutumia kifungu cha maandiko kuthibisha jibu lako.
16. Nadharia ya "immortality of the soul" – "Roho inayoishi milele" ina athari gani katika ufahamu wa Mpango wa Mungu wa wokovu?